



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MJI NEWALA



NTC/L.30/006/119

21/05/2022

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Newala anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa kazi ifuatayo:-

### MTENDAJI WA MTAZA DARAJA LA III – NAFASI (14)

#### SIFA ZA MWOMBaji:-

- Awe amefaulu kidato cha nne (IV) au sita (VI)
- Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada (cheti) "NTA Level 5" katika fani zifuatazo:-

Utarwala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii au Sayansi ya Jamii kutoka katika Chuo chochote kinachotambulika na Serikali

#### KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA MTAZA

- i. Kuwa Katibu wa Kamati ya Mtaa;
- ii. Mtendaji Mkuu wa Mtaa;
- iii. Mratibu wa utekelezaji wa sera na Sheria zilizotekelizwa na Halmashauri katika Mtaa.
- iv. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya maendeleo katika Mtaa;
- v. Msimamizi wa utekelezaji wa Sheria Ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa;
- vi. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama;
- vii. Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na Umaskini katika Mtaa;
- viii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
- ix. Kuandaa na kutunza rejestra ya wakazi wote wa Mtaa; na
- x. Kuwajibika kwa Mtendaji wa Kata

#### MSAHARA

Cheo cha Mtendaji wa Mtaa darajala III kina Mshahara wa TGS B kwa mwezi

#### MASHARTI YA UJUMLA

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa

- Mwombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma apitishe barua yake ya maombi kwa Mwajiri wake
- Mwombaji aambatanishe maelezo yake binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu
- Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti nya elimu na taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali
- *Testimonials, Provisional results, Statements of results* n.k hazikubaliki
- Waombaji waweke picha moja ya passport size katika barua zao za maombi
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **03/06/2022** saa tisa alasiri

Barua zote zitumwe kwa anwani iliyopo hapa chini

Mkurugenzi wa Mji  
 Halmashauri ya Mji Newala  
 186 Barabara ya Masasi  
 Mtaa wa Tupendane  
 S.L.P 39  
**63482 NEWALA**



Shamim D. Mwariko  
**MKURUGENZI WA MJI**  
**NEWALA**

#### **NAKALA**

- Katibu
- " Ofisi ya Rais
- Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma
- S.L.P 2320
- DODOMA**
- " Tovuti ya Halmashauri  
[www.newalatc.go.tz](http://www.newalatc.go.tz)
- " Mbao za Matangazo